Jina _____ Nambari _____

Sahihi ya Mtahiniwa _____

Tarehe _____

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
INSHA
JULAI / AGOSTI 2013
MUDA: SAA 1 ¾

TATHMINI YA PAMOJA KIDATO CHA NNE
WILAYA YA KATHONZWENI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA 2
INSHA
MUDA : SAA 2 ½

MAAGIZO

(a) Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu. Kisha tia sahihi yako na tarehe.

(b) Jibu maswali yote.

(c) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.

(d) Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

JUMLA	80	

Kijitabu hiki kina kurasa 9 zilizopigwa chapa

Geuza ukurasa

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ni dhahiri kwamba uharamia umechipuka kama desturi na mfumo wa maisha katika siku za hivi karibuni. Janga hili limeshamiri hususan pembeni mwa bara la Afrika Mashariki. Taarifa za uharamia zimetawala vyombo vya habari, kiasi cha kwamba haipiti siku bila kuripotiwa visa vipya vya matendo haya mabovu ambayo yanaweza tu kumithilishwa na uhayawani. Matukio haya yamewalimbikizia mabaharia na nchi husika, simanzi na masaibu yasiyoweza kutiwa kwenye mizani.

Yumkini tatizo hilo halitokei pasi na kumotishwa na kitita kikubwa cha fidia kinachodaiwa na maharamia hawa. Aghalabu, suala hili lahusishwa pakubwa na azma na ari ya kuendeleza ujambazi wa kimataifa sawia na ulipuaji wa bomu mijini Nairobi na Dar es Salaam mnamo Agosti 7, 1998, na tukio la September 11, mwaka wa 2001 kule Marekani. Maafa na uharibifu wa mali si hoja, la mno kwa maharamia ni kutosheleza matakwa yao. Kwa upande mwingine, ukosefu wa tawala – wajibika katika maeneno kunakotokea unyama huu ni thibitisho tosha la mazingira yanayowezesha na kuruhusu kuchipuka kwa janga hili.

Mchipuko wa baa la uharamia umelengwa jamii ya kimataifa ambayo ni mhudumu mkuu wa harakati kusitisha majanga makubwa kama vile njaa, umaskini na magonjwa yaliyosheheni pakubwa barani. Bila shaka, hili ni suala linaloshawishishwa na 'kinyume mbele.' Maharamia wanatishia utangamano wa kimataifa wanapotibua usafiri wa abiria na shehena zinazoelekezwa sehemu tofauti ulimwenguni.

Matumizi ya kidiplomasia na mashauriano hayaelekei kuzalisha matunda katika juhudi za kudhibiti uharamia. Zaidi ya hayo, matumizi ya nguvu yahusishayo mashambulizi pamoja na maharamia kufunguliwa mashtaka nchini Kenya na Ufaransa kunaelekea kupiga jeki juhudi za uharamia ulimwenguni. Aidha, utawala wa nchi kunakochipuka uharamia haujajizatiti kuharamisha doa hili linalotisha ustawi wa kimataifa.

Mathalan, ni jambo lisilopingika inapobainika kuwa uharamia umedumaza biashara ya kimataifa hali inayochangia upungufu na ucheleweshaji wa bidhaa muhimu zinazoendeleza ustawi wa uchumi. Dosari hii inaelekea kukwamiza mojawapo ya maendeleo ya milenia yanasisitiza uimarishaji na ushirikiano wa maendeleo ya upanuzi wa masoko ulimwenguni. Harakati za kitalii katika kanda ya Mashariki ya bara la Afrika zimehujumiwa. Na itakumbukwa bayana watalii hawasafiri tu kwa ndege bali hata kwa meli.

Jitihada za kuweka laini za mawasiliano chini ya bahari ili kurahisisha na kupunguza gharama za mtandao ulimwenguni ni ndoto ambayo haijatimia hadi hivi sasa, kufuatia juhudi za maharamia katika bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa hali hii, mawasiliano mepesi na nafuu yasitarajiwe hivi karibuni. Licha ya hayo, shughuli za uvuvi na biashara nyinginezo kwenye kanda ya mwambao zimetiliwa shaka si haba. Itabidi mikakati na suluhisho la kudumu liweze kupatikana ili vitendo vya uharamia viweze kusitishwa.

Maswali

(a) Kwa nini uharamia umetamalaki ulimwenguni? (alama 3)

_____

_____

_____

_____

(b) Fafanua dhana ya ‘kinyume mbele’kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

2

(c) Uharamia unaelekea kumtia hofu mwandishi. Fafanua. (alama 3)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(d) Thibitisha kuwa Kenya imeathirika pakubwa kutokana na vitendo vya uharamia. (alama 4)

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa kifungu. (alama 3

(i) Uharamia _____

(ii)Mtandao _____

(iii) Mwambao _____

2. UFUPISHO

Soma taarifa hii kisha ujibu maswali.

Kuna wataalamu siku hizi wanaosema kuwa jela si pahala pa adhabu bali pa matibabu. Yaani madhumuni ya kumtia mhalifu jela isiwe kumwadhibu kwa makosa aliyofanya bali iwe kumtibu na kujaribu kumrekebisha tabia yake ili awe raia mwema.

Zamani wahalifu waliadhibiwa kwa mujibu wa makosa waliyoyafanya. Mhalifu aliyefanya makosa madogo madogo alifungwa lakini mtu aliyeua naye aliuawa. Sasa wataalamu wanatuambia kuwa mhalifu akiadhibiwa anapokuwa kifunguno, basi akitoka hurejea tena kufanya uhalifu. Madhumuni ya kumtia jela iwe si kumwadhibu bali kumfunza tabia njema. Wanatuambia kuwa makosa afanyayo mhalifu yanatokana na matatizo ya jamii kwa jumla, nayo ni matatizo kama ya umaskini, msongamano wa watu katika miji, ugomvi manyumbani baina ya wazazi na kadhalika. Kwa hivyo, kwa mujibu wa wataalamu hawa, kosa afanyalo mhalifu si kosa lake pekee bali ni kosa la jamii nzima.

Jitu lililozoea kuua halioni kitu kumpiga kisu mwanamke njiani au kumpiga mtarimbo au rungu la kichwa na kumyang'anya kila alicho nacho. Siku hizi, jitu kama hili baadhi ya wataalamu husema lisiuawe, lifungwe maisha tu. Lakini 'kifungo cha maisha'ni kama tunavyokijua. Muuaji hufungwa pengine miaka kumi tu kisha husamehewa muda uliobaki. Hapo tena huwa huru ama kuifichua mali aliyoiiba na kuistarehea raha mustarehe au kurejea tena kufanya uhalifu.

Haya ni kinyume kabisa na mambo yaliyokuwa zamani. Aliyeua aliuawa kwa hivyo watu waliogopa kuua. Raia na pia askari waliokuwa wakiwasaka wahalifu walinusurika vifo kwani wahalifu wengine walichukua silaha za hatari kama bastola na bunduki.

Sasa wale wahalifu wabaya sana – mijizi, minyang'anyi na wauaji ndio wanaotukuzwa. Magazeti huwashawishi makatili hawa na kuwapa mapesa chungu nzima waeleze maisha yao ya kikatili. Magazeti haya sasa ndiyo yanayopata wasomaji wengi. Pia wachapishaji vitabu vya hadithi zinazohusika na uhalifu, biashara zao zinazidi kustawi. Kadhalika sinema zinazoonyesha picha za ukatili; wizi na mauaji hujaa watazamaji wanaoshangilia uhalifu ufanywao.

Wahalifu kwa upande mmoja wanatukuzwa na masinema, vitabu na magazeti na kwa upande mwingine "haki" zao zinapiganiwa na baadhi ya wataalamu. Watu wanaowalaani wahalifu ni wale waliohasirika tu na kuteswa na wahalifu. Baadhi yao hata kulaani hawawezi kwa sababu wameshauawa, hawana tena kauli.

Maswali

(a) Fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu kwa maneno 50.

(alama 7
Utiririko

1)

Matayarisho

_____

_____

Nakala safi.

4

(b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno kati ya 45 – 50 (alama 8)
Utiririko

2

Matayarisho

Nakala safi

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

3. MATUMIZI YA LUGHA.

(a) Taja sauti mbili za nazali. (alama 2)

(i) _____

(ii) _____

5

(b) Ainisha viambishi katika kitenzi. (alama 3)
Aliowaandalia

_____

_____

_____

_____

_____

(c) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi. (alama 2)

(i) Paka _____

(ii) Toroka _____

(d) Ainisha viwakilishi katika sentensi . (alama 2)

Vya mlevi huliwa na wengine.

_____

_____

_____

_____

(e) Yakinisha sentensi hii. (alama 3)

Nisipomwona leo jioni sitamlipa deni yake.

_____

_____

_____

_____

_____

(f) Andika kwa msemo wa taarifa. (alama 2)

“Lo! kweli umemtendea unyama huu wote? alishangaa.

_____

_____

_____

_____

(g) Tunga sentensi ukitumia ‘filisi’ katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(h) Eleza matumizi ya ‘na’ katika sentensi hii. (alama 3)

Hamisi na Halima wanaadhibiwa kwa sababu waliandikiana barua.

_____

_____

_____

_____

(i) Eleza matumizi ya kiambishi kilichopigiwa mstari. (alama 2)

Sisi ni waalimu na twawashauri msomeni kwa bidii.

_____

_____

_____

_____

(j) Andika kwa udogo (alama 2)

Ng'ombe aliyeanguka mtoni swalivunjika mguu na pembe.

_____

_____

_____

_____

(k) Andika kinyume cha sentensi hii . (alama 2)

Mjomba aliingia ndani na kumfungia kaka nguo haraka.

_____

_____

_____

_____

(l) Bainisha ngeli za nomino hizi. (alama 2)

Nyavu _____

Chai _____

(m) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali ulizopewa. (alama 4)

Kutenda	Kutendewa	Kutendata
Suka	_____	_____
Kama	_____	_____

(n) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mchoro wa matawi. (alama 4)

Tajiri aliyewahudumia wananchi amepewa tuzo maridadi.

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

(o) Bainisha aina za virai katika sentensi hii. (alama 3)
Mtoto wao mchanga amelala kitandani chali.

_____

_____

_____

_____

_____

(p) Ainisha shamirisho na chagizo katika sentensi
Waimbaji waliimba wimbo polepole. (alama 1)

_____

_____

_____

_____

(q) Eleza matumizi ya po katika sentensi hii. (alama 1)
Sijui alipohamia lakini ajapo mwulize.

_____

_____

_____

_____

4. ISIMU JAMII. (alama 10)

(a) Makosa ya lugha hutokea vipi ? (alama 2)

_____

_____

_____

_____

(b) Eleza kwa ufupi jinsi mambo yafuatayo yanavyochangia makosa katika lugha ya Kiswahili. Toa mfano.

(i) Athari za lugha ya kwanza. (alama 2)

(ii) Kutofahamu kanuni za sarufi. (alama 3)

(iii) Makosa ya lugha kimakusudi. (alama 3)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs